## FAIDA ZA ALAMA YA UBORA YA "tbs"

### Kwa Mteja/Mlaji

- Humthibitishia kuwa bidhaa husika inafaa kwa matumizi husika;
- Huwezesha kupungua kwa bei ya bidhaa kutokana na ushindani;
- Humhakikishia usalama wake kiafya na katika matumizi;
- Huongeza ubora wa bidhaa;
- Hulinda mazingira yake.

### Kwa mzalishaji

- Humpa uwezo mkubwa zaidi wa kushindana sokoni;
- Humpatia wateja zaidi;
- Humwondolea usumbufu wa kupima bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya mnunuzi;
- Humkinga dhidi ya ushindani na bidhaa duni zisizo na ubora.

## MAABARA

TBS ina maabara tisa zenye vifaa vya kisasa na wataalamu wa kutosha. Maabara hizo ni:

- Maabara ya Kemia;
- Maabara ya Uhandisi wa Umeme;
- Maabara ya Uhandisi Mitambo;
- Maabara ya Uhandisi wa Ujenzi;
- Maabara ya Kemia ya Chakula
- Maabara ya Pamba, Ngozi na Nguo;
- Maabara ya Mikrobiolojia;
- Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji.
- Maabara ya Jotoridi, Umeme, Muda na Masafa
- Maabara ya Tungamo na Vipimo vinavyohusiana
- Maabara ya Urefu
- Maabara ya Kemikali

Kwa maelezo zaidi,wasiliana nasi kwa anwani zifuatazo:

### MKURUGENZI MKUU

Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
S.L.P. 9524, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2450298 / 2450206/2451763-6
Hotline: +0800 110 827/ Nukushi: + 255 22 2450959
Baruapepe: info@tbs.go.tz/ Tovuti: www.tbs.go.tz
Malalamiko: malalamiko@tbs.go.tz

### OFISI ZA KANDA:

**NYANDA ZA JUU KUSINI**
(Iringa, Mbeya, Njombe and Songwe)
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S.L.P. 1674 Mbeya, Tanzania
Simu: 025 2502848 / Nukushi: 025 2502848

**KANDA YA ZIWA**
(Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu and Shiyanga)
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S.L.P. 1814 Mwanza, Tanzania
Simu: 028 2505044 / Nukushi: 028 2505044

**KANDA YA KASKAZINI**
(Arusha, Kilimanjaro, Manyara and Tanga)
Ngorongoro Tourist Center, Ghorofa ya 6
S.L.P. 2399 Arusha, Tanzania
Simu: 027 2520143 / Nukushi: 027 2520143

**KANDA YA KATI**
(Dodoma, Singida and Tabora)
Kambarage Tower, Ghorofa ya 6
S.L.P 2956, Dodoma, Tanzania
Simu: 026 2320310 / Nukushi: 026 2320310

**KANDA YA KUSINI**
(Lindi, Mtwara and Ruvuma)
Jengo la PSSSF, Sokoine House, Ghorofa ya 3
S.L.P 1396 Mtwara,Tanzania
Simu: 023 2334477 / Nukushi: 023 2334477

**KANDA YA MAGHARIBI**
(Katavi, Kigoma and Rukwa)
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S.L.P 1276 Kigoma,Tanzania
Simu: 028 2804023 / Nukushi: 028 2804023

**KANDA YA MASHARIKI**
(Dar es Salaam, Morogoro na Pwani)
Jengo la PSSSF (Commercial Complex) Ghorofa ya 4
S.L.P 9425, Dar es Salaam

TBS_Tanzania tbs_viwango TBS Viwango TV

TANZANIA BUREAU OF STANDARDS tbs

# Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

# KWA UFUPI



## UTANGULIZI

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ni Shirika la Umma chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara lililoundwa chini ya Sheria ya Bunge Nambari 3 ya mwaka 1975 na kurekebishwa chini ya Sheria Namba 1 ya mwaka 1977. Sheria ya Viwango ya mwaka 1975 ilifutwa na nafasi yake kuchukuliwa na Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 kwa lengo la kulipa shirika nguvu zaidi kisheria kutekeleza majukumu yake.

## MAJUKUMU YA TBS

*TBS ina majukumu mengi, lakini makuu ni haya yafuatayo:*

a) Kutayarisha viwango vya kitaifa katika sekta zote za uchumi, biashara na huduma.
b) Kutekeleza viwango katika viwanda, biashara na huduma.
c) Kuboresha bidhaa zinazozalishwa nchini kwa ajili ya masoko ya ndani na nje.
d) Kuelimisha umma juu ya masuala yote yanayohusu uwekaji na usimamiaji wa viwango pamoja na uthibiti wa ubora wa bidhaa viwandani.
e) Upimaji wa sampuli kwa lengo la kuthibitisha ubora.
f) Kuthibitisha usahihi wa vipimo vinavyotumika viwandani na katika sekta za huduma na biashara.
g) Ukaguzi na usajili wa majengo / maeneo kama machinjio, mabucha, maduka makubwa (supermarkets), maduka ya chakula na vipodozi, wanaopika vyakula kwenye masherehe (carterers), mahoteli, migahawa, maghala na maeneo ya uzalishaji.
h) Usajili wa vyakula na vipodozi.

## VIWANGO VYA TANZANIA

Viwango vya Tanzania ni Viwango vya Kitaifa vilivyokwishawekwa au vitakavyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Viwango vikielezea kanuni za uzalishaji, uhifadhi na ufungashaji wa bidhaa.

Mpaka sasa TBS imeishaweka viwango zaidi ya 1600 katika nyanja za Kilimo na Chakula, Ngozi, Kemikali, Nguo, Uhandisi Mitambo, Uhandisi Ujenzi na Uhandisi Umeme.



*Kamati ya kitaalamu ikitayarisha kiwango*

## UTEKELEZAJI WA VIWANGO

### 1. Ukaguzi bandarini

TBS huchukua sampuli wakilishi kabla bidhaa hazijapakuliwa katika bandari na mipaka yetu ili kuthibitisha ubora wa bidhaa husika. Bidhaa bora tu ndizo huruhusiwa kuingia nchini.

### 2. Ukaguzi wa kushitukiza sokoni

TBS hukagua bidhaa kwa kushitukiza sokoni bila kumpa taarifa muuzaji. Bidhaa zisizofaa huharibiwa na muuzaji huchukuliwa hatua mbalimbali zikiwemo faini na kushitakiwa mahakamani.

### 3. Usajili wa Bidhaa na Majengo

TBS hufanya usajili wa bidhaa za vyakula na vipodozi vinavyozalishwa nje ya nchi na kuingizwa nchini. Bidhaa zinazokidhi viwango tu ndizo husajiliwa na kuruhusiwa kuingizwa nchini.

Aidha, TBS husajili majengo yanayotumika kuhifadhi, kuuzia na kusambaza vyakula mfano maghala, migahawa, maduka ,mabucha, mahoteli n.k.
Majengo yanayokidhi vigezo vilivyowekwa husajiliwa na kuruhusiwa kutumika kwa biashara za vyakula na vipodozi.

## FAIDA ZA VIWANGO

- Huweka usawa katika uwanja wa biashara;
- Huondoa mkanganyiko kuhusiana na bidhaa;
- Husaidia kufungua masoko zaidi;
- Hurahisisha biashara baina ya nchi na nchi;
- Hutoa uhakikisho wa ubora, usalama, kuaminika na ufanisi;
- Huipa serikali urahisi wa kuunda sheria zinazohusiana na masuala ya afya, usalama na uhifadhi wa mazingira;
- Hulinda afya na usalama wa walaji/watumiaji wa bidhaa mbalimbali.